

UNO

# YAAMURU URENO TOA UHURU

1 Aug, 63

UNO — NEW YORK, Jumatano.

**B**ARAZA LA USALAMA LA UMOJA WA MATAIFA LEO LIMEPITISHA AZIMIO LA KUITAKA NCHI YA URENO KUMALIZA KABISA UBAYA UNAOFANYIKA KATIKA NCHI ANAZOZITAWALA KATIKA AFRIKA, NA KUANZA KUZITAYARISHA NCHI HIZO ZIPATE UHURU WAKE.

Upigaji kura wa azimio la Baraza hilo lenye watu 11 lilionyesha kwamba mataifa 8 yanapendelea na mataifa matatu hayakupiga kura kabisa.

Mataifa ambayo hayakupiga kura ni Amerika, Uingereza na Ufaransa. Azimio la kuitaka nchi ya Ureno itoe uhuru kwa nchi za Afrika lilitiwa kwenye agenda ya mkutano na mataifa yote ya Kiafrika na Kiasia.

Azimio hilo pia lilitaka nchi zote zichukue hatua ya kumzuia Mreno asipate silaha na vyombo vingine vya kivi-ta, kwasababu Mreno huzitumia sana hizo kwa 'kuwakandamiza' wananchi wa huko.

Ingawaje azimio hilo lilipunguzwa makali kuliko ilivyo-

kuwa mwanzo lakini nchi ya Amerika imesema kuwa kuli-kuwamo vifungu ambavyo nchi hiyo ilivipinga.

Wakati wa majadiliano Wajumbe wa Kiafrika walisema kwamba silaha zilizotolewa na nchi ya Amerika pamoja na nchi nyingine za Ulaya zimetumiwa kuwauwa watu wanaopinga utawala wa kibeberu wa Mreno.

Nchi za Afrika zilizosaidia kuandika azimio hilo zimesema kwamba zilijua nchi tatu hizo zitapinga wakati wakupiga kura.

## Mambo matano

Katika azimio huo mambo matano yaliwekwa mbele.

1. Kuchukizwa na Mreno kwa kuendelea kukataa au kutii maazimio ya umoja wa mataifa.

2. Kwamba hali iliyoko katika nchi za Mreno zilizoko Afrika zinaweza kuharibu amani katika Afrika.

3. Mreno anahitajiwa upesi akubali haki za wananchi kupata uhuru wao, na kwamba waanze majadiliano na viongozi waliochaguliwa na raia ili kuwapa uhuru wao.

4. Na kuziomba nchi zote kumnyima Mreno msaada wa namna yeyote ambao utamfanya azidi kuendelea kuwakandamiza wananchi na kuwanyima silaha kwa shabaha hii.

Azimio hilo pia limemwomba Mwandishi Mkuu, U Thant kuona kuwa azimio hilo linatimizwa na kwamba mwisho wa mwezi wa Septemba atoe ripoti yake.

Azimio hilo lilitolewa na nchi za Ghana, Morocco na Phillippines ambao ni wanachama wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.